**SECONDARY END TERM 1 EXAM 2017**

**KISWAHILI 102/3**

---

**Prepared by Schools Net Kenya (SNK) | P.O. Box 8076 – 00200, Nairobi**

**|Tel: +254202319748 | +254 711 88 22 27**

**Website: www.schoolsnetkenya.com**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com**

**KISWAHILI 102/3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**SEHEMU YA KWANZA (A)**

**KIDATO CHA TATU**

**1. USHAIRI**

**(a) Mambo muhimu**

Mkulima ambaye ni nguzo ya africa ni kama mtumwa
Anateseka ana huzuni
Baadaye matumaini yanaweza kuisha
Kuna siku ambapo atafahamu haki yake na adai
Wanaomtesa wataadhibiwa
Mwenye bidii
Hana matumaini
Umaskini
Hasira/hamaki (4x1=4)

**(b) Tamathali za usemi**

Tashbihi- kama kuni/ kama habari
Kweli kinzani- mtumwa wa watumwa waliyoridhiwa nguzo tena anatabika kwa njaa
Tashihisi- pumzi zilizozima taa za afrika
Mkono ulommumbua
Uso ukifuka hukata
Semi- moyo mzito, kufa ganzi
Istiara- taa ya maisha
Jazanda- ghadhabu ya kiu/nguzo ya afrika/taa
Mdokezo-mtazameni
Balagha- ubeti wa tano (4x1=4)

(c) Umbo la shairi
(i) Beti sita
(ii) Mishororo hajitoshelezi/hailingani/sakarani
(iii) Ushairi huru, mizani hailingani. Kila mshororo una idadi tofauti ya mizani
(iv) Vina vya nje vipo katika baadhi ya ubeti

(d) Matumizi ya kihisishi
Mshangao, huruma ya masikitiko kuwa aliye nguzo ya afrika ni mtumwa wa watumwa, kuteka makini ya msomaji(hisia)
(e)(i) Wakati (mkulima) atakapozinduka na kudai haki yake kwa hasira
(ii) kutuliza hasira za mkulima matakwaa /matatizo yake hate kama ni kidogo
(f)(i) Tambo-
(ii) ulokomaa-
(iii) kumtoweka-

**SEHEMU YA B**
**2 . Uzembe na mapuuza hiathii maendeleo ya nhi. Thibitisha**
1. Nasaba bora alipuuza usafi wa madhari yake k.m Magugu yamemea hata ndani ya mabaki ya tinga ti nga, mafuta meusi yalikuwa yamezagaa chini kotekote. Nyumba ya kuegesha magari ilikuwa katika hali mbaya.
(ii) Nyumbani mwa Nasaba – masofa yalikuwa yamezeeka na kurauka
(iii) Zuhura alijiachilia hadi akawa mchafu wa kupindukia na kunenepa kupita na sura na siha yake kuharibika.
(iv) Chai- ilipoletwa wakati Majisifu alifika kwa Nasaba ilikosa maziwa kwa sababu ya Amani kuwa kifungoni na ng'ombe kukosa mkamaji.
(v) Nzi-Nzi mkubwa alijichoma ndani mwa kikombe cha chai cha Nasaba Bora
(vi) Panya- Walikimbia ovyo ovyo katika nyumba ya Nasaba na katika kibanda cha Amani walipiga kambi pale
(vii) Majibwa- Jimmy, jibwa la mtemi lilikosa matibabu na kupata ugonjwa wa mbwa Jimmy aliwauma watu wengi kwa mfano DJ na kumwambukiza ugonjwa.
(viii) Gari- Nasaba alununua gari lake aina ya Nissan Sunny na kisha kuliacha kuharibika
(ix) Tinga tinga- lilifanya kazi vizuri wakati wa majununi la Massey Fergusson liliachwa kuharibika na kuwa kutoweza kufanya kazi tena.
(x) Majisifu- aliacha kufanya kazi yake ya kufunza na kuishi kwa mama Ntilie kulewa pombe. Akiwa mhadhiri aliiba miswada ya waandishi wengine.
(xi) Wanguzi- Katika Zahanati ya Nasaba Bora walikataa kumtibu uhuru na kusababisha kifo chake.
(xii) Wananchi wa Baraka walishindwa kumwokoa Imani kwa sababu ya ya uoga na kufanya unyanyasaji kuendelea
(xiii) Usafi- Nasaba alisema kuwa si vizuri kuwa msafi sana nah ii ndio sababu aliwacha kunadhifisha mandhari.
(xiv) Amani- aliwalaumu wananchi kwa kukosa kumwondoa Mtemi na kuwa waoga hadi anawakalia na kufanya maisha yao yawe magumu.

**3. (a) Muktadha**
(i) Msemaji ni mtemi
(ii) Alikuwa anawaambia Imani na Amani
(iii) Walikuwa nyumbani kwake Mtemi nasaba bora
(iv) Walikuwa wanatafuta kazi (4x1=4)
**(b) Sifa za mtemi**
1. Alifunga Imani na Amani kwenye seli bila hatia
2. Aliamrisha askari wawapige
3. Kunyakua Ardhi kimabavu kutoka kwa babuye Amani Chirchir (Yusuf)
4. Hakujali na hakumshughulukia DJ baada ya kuumwa na mbwa wake.
5. Alimkataa mtoto uhuru aliyetupwa mlangoni pa Amani

6. Aliwapata Amani na Imani kwa gari walipokuwa wanampeleka Uhuru hospitalini
7. Alikandaniza mkewe- hakupenda mkewe hakumtunza
8. Hakutoa mahitaji ya nyumbani kama mume
9. Kuamrisha kumtia kizuizini kwa matuko Weye kwa kumsuta kwenye sherehe za uhuru
10. Anadhulumu mtoto wa shule lowela kimapenzi (5x2=10)

(iii) Dhiki zilizowaakumba wazungumziwa

**1. Amani**

(a) Kupoteza mswada wake wa kidagaa kimemwozea
(b) Kupoteza shamba la wazazi wake na kukosa makao
(c) Kufungwa bila hatia
(d) Masomo yake kukatizwa chuo kuku kwa visingizio vya siasa
(e) Dhuluma kutoka kwa mwajiri, kuachwiwa mtoto kulea asiye wake
(f) Kuishi katika makazi duni (kibanda) (zozote 3x1=3)

**Imani**

(a) Kuuwawa kwa mamake
(b) Wazazi wake kupokonywa shamba
(c) Kutorokwa na nduguze baada ya mgogoro wa shamba
(d) Dhiki ya kutafuta kazi kwenye Mtaa wa matajiri
(e) Dhiki ya kulea mtoto Uhuru asiyewake
(f) Dhiki ya kuwalea watoto walemavu
(g) Kufungwa bila hatia (zozote 3x1=3)

**4. (i) Muktadha**

(i) Maneno haya yamesemwa na Bili
(ii) Alikuwa akimwambia Meya
(iii) Wakiwa ofisini mwa Meya
(iv) Bili alikuwa anamshauri Meya akubali kuenda kortini na kukiri juu ya kandarasi aliyotoa kwani Bili anaamini kuwa hakimu anatoa uamuzi wa mwenye kandarasi kulipwa fidia (4x1=4)

(b) Tumbo limewekwa mbele

1. Madiwani wanaomuunga Meya mkono wanatuzwa kwa vyeo na marupurupu. Wanaongezwa mishahara, hawawajali wananchi wafanyi kazi hawajalipwa mishahara kwa miezi kadha

(2) Kamati –Kamati kuundwa na madiwani walio na ushauri mkubwa kuwekwa katika kamati kisha walipwe vizuri. Hata baada ya kuambiwa na Diwani III kuwa haiwezekani kwani wafanyikazi hawajalipwa, wanalazimisha kuongeza kodi ili kupata pesa hizo,

(3) Meya anapinga kumfurusha mwenye kandarasi. Bili anampa njia ya kujifaidi kuwa waweza kumlipa fidia na hivyo mwenye kandarasi ampe Meya hongo.

Baraza ndilo linalipa na huku watu wanakufa kwa sababu ya kukosa dawa.

(4) Meya anataka kujenga uhusiano bora na nchi zingine kwa mapokezii kwa wageni, anatumia pesa nyingi na ilhali wananchi hawana mahitaji ya kimsingi ya chakula na dawa, mvinyo kutoka urusi, divai kutoka ufaransa na vyakula kutoka tamaduni zote za duniani
(5) Meya kujinyakulia vipande vya ardhi, kisha kuviuza ili kupata pesa za matumizi ya starehe –prime plot. Meya amenyakua vipande vinane vya ardhi, kuuza vitatu na kubakisha vitano. Alimpa Bili vipande vinnne anamhimiza auze viwili
(6) Diwani III anasema kuwa Umeya hauana pesa nyingi lakini ofisi ndiyo ina mianya mingi ya kujitajirisha
(7) Meya amenenepa kwa sababu ya kula sana ilhali raia wamekondeana, watoto kama Dadavuo wana utapia mlo. Wananchi hawana chakula cha kutosha
(8) Madiwani kuongezwa mishahara mwezi hu na umebakisha siku mbili. Baraza lenyewe halina pesa kwa sababu wafanyi kazi wamegoma na kodi haitolewi. Kila wakati madiwani wanakutana ni njama ya kuongezwa mishahara. Kila wakati wanaipa nyongeza hiyo jina k.m overtime , marupurupu.
(9) Wanapokosa cha kuiba wanapanga, kuiba fimbo ya Meya , fimbo hii hutengenezwa kwa dhahabu kuiuza na kisha kuwasingizia wafanyi kazi
(10) Badala ya kusafisha mji, wanapuuza. Uvundo umekolea kils mahali na umewaalika wageni kufika kujionea maendeleo (zozote 8x2=16)
5. Ufisadi unaendelezwa na Baraza eleza
(i) Kila wakati Meya na wenzake kusema nchi ni changa na huku wanaiba pesa na malighafi. Pia kuwatwika wananchi mzigo wa kugharamia kil akitu kama matibabu.
(ii) Mfumo wa kugawana gharama unawafinya maskini wasio na pesa na kuwanenepesha viongozi. Kuna kugawana gharama lakini hakuna huduma.
(iii) Bei na vitu muhimu kama mafuta taa kupanda na huku wananchi wanakatazwa kukata miti
(iv) Gharama ya juu ya maisha. Maisha magumu mahitaji kupanda. Mshahara unabaki hivyo tu wa chini kwa raia
(v) Madiwani wanaomuunga Meya mkono wanatunzwa kwa vyeo na marupurupu
(vi) Madiwani wanataka kuongezwa mishahara ndipo kila wakati wafanye kazi vizuri
(vii) Meya anapanga kumfurusha mwenye kandarasi Bili anampa anampa njia ya kujifaidi kuwa waweze kumlipa fidia na huyo mwenye kandarasi ampe meya hongo
(viii) Mapokezi kwa wageni- anatumia pesa nyingi ilhali wananchi hawana mahitaji ya kimsingi ya chakula na dawa. Mvinyo kutoka urusi, divai kutoka ufaransa na chakula kutoka tamaduni zote duniani
(ix) Hali ya maisha ni chini sana, lakini ana pesa nyingi kuuza vipande vya ardhi alivyoiba kutoka kwa baraza –prime plot
(x) Wizi wa ardhi- Meya amenyakua vipande vya ardhi kuuza vitatu na kubakisha vitano. Alimpa Bili vipande vine, anamhimiza auze viwili.
(xi) Meya kukubali amefanya makosa ya kukatiza kandarsi, kisha amlipe na mwenye kandarasi ampe hongo. Barasa ndilo la kulipa si Meya.
(xii) Diwani III anasema kuwa Umeya hauna pesa nyingi lakini afisi ndiyo ina mianya mingi ya kujitajirisha
(xiii) Madiwani kuongezwa mishahara mwezi hu na umebakisha siku mbili. Baraza lenyewe halina pesa kwa sababu wafanyi kazi wamegoma na kodi haitolewi.
(xiv) Kila wakati madiwani wanakutana ni njama ya kuongezwa mishahara. Kila wakati wanaipa nyongeza hiyo jina k.m overtime , marupurupu.
(xv)Wanapokosa cha kuiba wanapanga, kuiba fimbo ya Meya , fimbo hii hutengenezwa kwa dhahabu kuiuza na kisha kuwasingizia wafanyi kazi (10x2=20)

**SEHEMU YA D**

**HADITHI FUPI : DAMU NYEUSI**

6.Wanafunzi wazungu wanakosa nidhamu na utu na kumuuliza Fikirini maswali ya kuudhi, km ikiwa kwao wanatembea uchi, wanajipaka lami ndipo wawe weusi, mji mkuu wa afrika ni upi, kama wanaishi kwa mti kama tumbili, kama wasichana wa kwao walikeketwa n.k
(ii) Wahadhiri wa vyuo vikuu vya ng'ambo kuwa na mapendeleo na kunyima Fikirini alama. Wahakikisha amepata alama za chini
(iii) Wazungu kutoamini Mwafrika amesoma na kuelewa kiingerereza ndipo wanamuuliza Fikirini kama anajua kiingereza wakati alikuwa amezingirwa na polisi.
(iv) Polisi walipoitwa eti Fikirini anaonyesha uchi wake, walifika wengi kwa magari na huku ni kama alikuwa jambazi sugu. Waliamini ni mhalifu kwa sababu ya rangi ya ngozi yake.
(v) Alilazimika kusoma zaidi ya shabaha iliyomleta kusoma tabia za wazungu, kujibu maswali yao ya kijinga na kusoma tabia za wamerekani weusi.
(vi) Hali ya anga ni tofauti sana na ya Afrika mashariki. Kuna theluji nyeupe kama wenyeji na baridi ya ajabu. Fikirini anavalia nguo nyingi lakini wapi baridi ilipenya ndani.
(vii) Wakati wa joto kuna joto jingi sana ambalo linamfanya Fikirini kukosa raha.
(viii) Fikirini alikuwa na tamaa ya vyakula vya nyumbani –ugali mlenda, matoke, muhogo, wali, pilau. Pombe za kienyeji kama gongo waraji an chang'aa. Huku ughaibuni chakula hakikuwa na ladha wa kueleweka.
(ix) Fikirini alikosa raha ya kwao na wasichana wanaopendeza na wenye roho safi, huko ugenini ni majamabazi hatari kama Fiona
(x) Fikirini alipoenda dukani kununua vitu alifuatwa na askari aliyedhania kuwa alikuwa ni jambazi na alitaka kuiba vitu.
(xi) Fikirini aliachwa na basi ambalo lilikuwa linaendeshwa na mzungu kwa sababu alishukiwa kuwa jambazi
(xii) Fikirini alipokuwa anavuka barabara taa zikiwa nyekundu, alishikwa na kushtakiwa. Wazungu walipovuka taa zikiwa nuekundu, waliachwa wafanye hivyo bila kuulizwa lolote
(xiii) Upweke- Kila wakati alikumbuka nyumbani na kutamani kurudi huku, alikumbuka vyakula, wasichana, vinywaji na maneno ya Rais Moi. Alitamani utajiri wa upendo wa kwao.
(xiv) Chakula cha ughaibuni kulikuwa hakipendeki. Fikirini alipokuwa anaingia mkahawani alikumbuka chakula cha kwao. (10x2=20)

**SEHEMU YA E**
**FASIHI SIMULIZI**
Ngano za mtanziko

(i) Hukuza uwezo wa kupima mambo na kuamua kuteua lililo muhimu

(ii) Hukuza uwezo wa kufadhiliana na kufikia uamuzi mwafaka

(iii) Huonya dhidi ya kutenda bila kiwaza kwa kina

(iv) Huadilisha

(v) Huburudisha

(vi) Huonya dhidi ya tabia hasi kama vile usaliti

(iii) Umuhimu wa maigizo ya watoto

- Hukuza undugu na ushirikiano tofauti za kijamii
- Hukuza ubunifu
- Huimarisha uwezo wa kukumbuka
- Ni kitambulisho cha jamii-watoto huigiza wayaonayo katika jamii zao
- Hupitisha maarifa
- Ni kiburudisho na njia nzuri ya watoto kupitisha muda
- Huwafunza watoto majukumu yao ya utu uzima
- Hupalilia vipaji vya uigizaji
- Huwapa watoto ujasiri na kujiamini (6x1=6)

**(iv) Fafanua sifa za Rara**

- Ni hadithi fupi nyepesi za kishairi ambazo husisimua
- Huweza kuandamana na ala za muziki
- Nyingi zilihusu koo tukufu/zilizotajika
- Hutolea kwa ...ya huzuni /kitanzia
- Masuala hufumbua na kudokezwa tu
- Lugha hujaa utendaji wa matukio
- Hushughulikia maswala ya kawaida na ibuka kwa mtindo usio rasmi
- Huwa na ucheshi wenye kinaya
- Baadhi huwa za kiburi japo nyingine ni za kweli (zozote 5x1=5)

**(v) Misimu**

- Huhufadhi siri
- Hukuza uhusiano bora
- Kuonea fahari kundi fulani kwa kuwaunganisha
- Hutambulisha kundi
- Huondoa makali kwenye lugha
- Huongeza ladha  katika lugha
- Huondoa urasmi
- Husawiri mpangilio wa jamii fulani kiuchumi *(zozote 4x1=4)*